# 'Lazima mifugo ilete tija'

DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

Tanzania inakadiriwa kuwa na mifugo milioni 33.9 ingawa kiuhalisia sekta ya ufugaji haina tija kubwa, si kwa wafugaji wala kwa taifa.

Karibu kila serikali iliyowahi kushika madaraka, imekuwa ikijaribu kuiinua sekta ya ufugaji ingawa hakujaonekana mafanikio makubwa, na sasa mdau mwingine, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), ameonyesha dhamira kuiwezesha sekta hii.

Katika mkutano wa wadau wa mifugo uliofanyika jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, benki hii inasema imejizatiti kuchagiza ukuaji wa sekta ya mifugo na nyama.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wapili kushoto), akisikiliza maoni ya wadau wa mifugo wakati wa mkutano uliofanyika Dar es Salaam hivi karibuni.

Mwenyekiti wa mkutano, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewahakikishia wadau wa ufugaji akisema TADB imeweka mkakati wa kuwafikia wafugaji wengi zaidi na kuwanufaisha kwa kuwapa fursa mbalimbali.

Kaimu Mkurugenzi wa Sera, Tafiti na Mipango wa TADB, Mzee Kilele, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji, Frank Nyabundege, anasema:

"Ninawahakikishia wadau kuwa tutaendeleza kasi ya kutoa mikopo na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo, hivyo kuiimarisha sekta hii ilete tija kwa wafugaji wenyewe na kwa uchumi wa taifa."

Hadi Agosti mwaka huu, TADB imekwisha kutoa mikopo ya moja kwa moja katika sekta ya mifugo yenye thamani ya Sh bilioni 23.8, ikiziwezesha AMCOS tano kupata ng'ombe wa kisasa, hivyo kuwanufaisha wafugaji 128; sekta inayohusiana na maziwa, benki imekwisha kutoa mikopo yenye thamani ya Sh bilioni 11.8, zikiwezesha ujenzi wa viwanda vinne vya maziwa vinavyozalisha lita 190,000.

"Wafugaji zaidi ya 60,000 wamenufaika na uwepo wa viwanda hivyo kwa kuviuzia maziwa," anasema Kilele.

Sehemu ya mikopo inayotolewa na TADB hutumika kuboresha miundombinu ya uzalisha kama ujenzi wa mabanda ya kisasa na viwanda vya kusindika nyama na maziwa.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Ndaki, anaahidi kusimamia utekelezaji wa mawazo ya wadau wa sekta ya mifugo katika kuiboresha na kutengeneza mazingira bora ya ufugaji.

"Niwatie moyo kwa kusema kuwa serikali ipo na itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wafugaji, kwani tunatambua mchango wao katika maendeleo ya uchumi na kutengeneza ajira kwa vijana," anasema.

Waziri amewashauri wadau kufanya ufugaji wa kisasa kwa kutilia maanani tiba na lishe ambazo ni silaha muhimu katika kuongeza uzito wa mifugo na kuwashawishi wanunuzi wa ndani na nje ya nchi.

"Ukosefu wa tiba na lishe duni huwafanya ng'ombe kuwa na uzito wa kati ya kilo 150 hadi 250 tu.

"Hii si sahihi kwa kuwa ng'ombe wa wenzetu huwa na kati ya kilo 500 hadi 600! Bado tuna kazi ya ziada kuzingatia lishe



Ufugaji wa kisasa na unenepeshaji ng'ombe ndiyo njia sahihi kuleta tija sekta ya uvuvi.

bora na tiba," anasema Ndaki.

Anasema serikali inafikiria kuanzisha mamlaka itakayosimamia malisho na masoko ya mifugo na mazao yake, itakayochagiza kuinua sekta kwa kupunguza migogoro na wafugaji kuhamahama.

Tayari serikali imeanzisha mashamba mawili ya malisho, ikijipanga kuanzisha mengine kadhaa kwa kushirikiana na halmashauri kwenye mikoa yenye idadi kubwa ya mifugo.

Kuhusu tatizo la maji, waziri amesema mabwawa makubwa na visima yatachimbwa maeneo yenye mifugo mingi na kusambaza maji kupitia 'mbauti'.

"Migogoro mingi husababishwa na uhaba wa malisho na maji, hasa nyakati za kiangazi. Hii ndiyo sababu ya wafugaji kuhamahama. Kwa kulitambua hilo, sasa tunawahamasisha wafugaji kupanda mbegu za malisho," anasema.

Ndaki ameihimiza TADB na taasisi nyingine za kifedha kuwawezesha wafugaji kwani uwekezaji ukifanyika kwa makini utazaa faida kubwa kwa wafugaji na taifa.

Katika hatua nyingine, waziri anaahidi kumaliza kabisa migogoro ya ardhi inayotokea kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Tayari sekta ya ufugaji, kwa mujibu wa Ndani, imeshaanza mazungumzo na wanunuzi kutoka nje ya nchi kuja kununua nyama inayozalishwa nchini.

"Mazungumzo yamefanyika na mataifa kama Marekani, Uarabuni na mataifa ya Ulaya kuja kununua nyama Tanzania," anasema.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na Mjumbe wa Bodi ya Chama cha Wafugaji Tanzania, Juma Homera, ameishauri Benki ya kilimo kuwawezesha vijana kutambua fursa zilizopo katika ufugaji.

"Natambua mchango na kazi kubwa inayofanywa na benki hii. Wenye kulalamikia uhaba wa ajira ni vijana. Kwa hiyo hawa wakizitambua fursa katika ufugaji, tatizo la ajira litapungua," anasema Komredi Homera.

Anasema upo umuhimu wa kuanzisha mamlaka rasmi kusimamia masuala ya mifugo, akiamini ndio utakuwa mwarobaini wa matatizo yote ndani ya sekta husika.

"Tukiwa na mamlaka kama hiyo tutauona mara moja ufanisi na tija katika ufugaji," anasema.

Jackson Kamkoto, Mwenyekiti wa Wafugaji Wilaya ya Karagwe, mbali ya kuwa na matumaini katika maazimio yaliyofikiwa, amezitaja sababu za ukosefu wa elimu kwa wafugaji, uhaba wa wataalamu na malisho kama changamoto kubwa zinazowakabili wafugaji.

"Matumaini yangu ni kwamba maazimio ya mkutano huu yatakwenda kubadilisha sekta nzima na kuwa na manufaa kwetu wafugaji na taifa kwa ujumla," anasema Kamkoto.

Matumaini ya wadau wengi wa sekta ya ufugaji ni kuiona TADB inaendeleza jitihada za kuinua sekta.

loka

natunda bure
nchi na kwamba
a zaidi ya miche
matunda ime-
wa kwa waku-

tuanze mradi huu
miche zaidi ya
ini katika msimu
haandaa miche
000 ambapo
800 wamenu-
amo taasisi za
dini, lengo letu ni
uwezo wanan-
mazingira na
a kiuchumi,"

Mkurugenzi wa Taasisi ya Doris Mollel, Doris Mollel akimkabidhi Spika wa Bunge, Job Ndugai kitabu baada ya kuzindua ajenda ya mtoto njiti jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Wetu).

swa

leleo ya kijamii
afanya wao na
dumia kuwa
zi bora.
i wa TGGA,
Qorro, alitoa
hana kujenga
ea kwani ni
apo ya mtu ku-
a kwa ambao
tika taasisi za

nyekiti wa
A Mkoa wa
e Mohindo,
o hayo yana-
shiriki zaidi ya
a 20 ya Tanza-
zibar ambao ni
sisi hiyo ngazi

# Uvuvi haramu Mtera waathiri wananchi

Na Frank Leonard, Iringa

UVUVI haramu katika Bwawa la Mtera wilayani Iringa umeporomosha kwa kasi kubwa uchumi wa wananchi wa Kata ya Migoli wanaotegemea biashara ya samaki kama moja ya vyanzo vyao vikuu vya mapato.

Diwani wa Kata ya Migoli inayopakana na bwawa hilo, Benito Kayugwa alisema hivi karibuni kwamba, uvivu huo umeharibu mazalia ya samaki na kusababisha uhaba wa samaki hali inayoyosababisha baadhi ya wananchi kuyakimbia makazi yao na kwenda kutafuta maisha sehemu nyingine.

"Migori ya sasa sio sawa na Migori ya miaka ya nyuma ambayo maisha na maendeleo ya wananchi wake wengi yalikuwa yakitegemea bwawa hilo kupitia uvuvi unaokubalika kisheria kwa kutumia nyavu kubwa ili kuwanusuru samaki wadogo wasipotee," alisema diwani huyo.

Alisema katika kukabiliana na uvuvi haramu, kata yake imeunda kikosi kazi chenye watu 64 kinachohusisha Mkuu wa Kituo cha Polisi Migoli na ofisa uvuvi kwa lengo la kuwakamata wavuvi haramu pamoja na zana zao haramu na kuwashughulikia kwa mujibu wa sheria kwani wanaochangia kuharibu mazalia ya samaki katika bwawa hilo.

Alisema takwimu za kati ya Julai, mwaka jana hadi Agosti, mwaka huu zinaonesha jumla ya nyavu haramu 11,538 zenye thamani ya zaidi ya Sh milioni 152 zilikamatwa na kuteketezwa kwa moto kama moja ya njia ya kupambana na uvuvi huo.

Hivi karibuni Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, alichoma moto nyavu haramu 80 zenye thamani ya Sh 13,814,000 zilizokamatwa kati ya Julai na Agosti, mwaka huu zikiwa zinatumiwa kufanya uvuvi haramu.

Moyo alisema, kumekuwa na tabia ya baadhi ya wavuvi kuvua samaki kwa kutumia njia haramu ambazo zimekuwa zikileta madhara kwa samaki na kuharibu mazalia yao hivyo kusababisha samaki kukosekana katika bwawa hilo.

Alizitaja nyavu zilizokamatwa kuwa ni pamoja na zile zinazotambuliwa kwa jina la timba, kokoro, gonga, kimila na nyavu chini ya inchi tatu na kuwataka wananchi kushiriki katika kampeni ya kutokomeza aina hiyo ya uvuvi.

"Serikali inatoa elimu ya usimamizi shirikishi wa kulinda rasilimali za uvuvi na kudhibiti uvuvi haramu na usafirishaji wa samaki wachanga kwa mujibu wa sheria ya uvuvi ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009," alisema na kuongeza kwamba mbali na makundi mbalimbali ya kijamii yanayozunguka bwawa hilo, zaidi ya wavuvi 249 wamepata elimu hiyo.

Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Methew Sanga, alisema kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu wavuvi 11 walikamatwa kwa uvuvi haramu, kati yao tisa waliachiwa huru baada ya kulipa faini na wengine wawili wanasubiri maamuzi ya mahakama kwa kuwa walikubali kufanya vitendo hivyo vya uvuvi haramu.

"Ili kuwasaka wavuvi haramu, serikali imetoa boti moja ya doria ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kuharakisha kampeni ya kuwasaka na kuwakamata wavuvi wanaojishughulisha na uvuvi haramu," alisema.

Wakati huo huo Moyo ametoa taarifa inayohusu wavuvi 12 kupoteza maisha na wengine 15 kujeruhiwa kati ya Februari, mwaka jana na Agosti, mwaka huu katika matukio ya kuvamiwa na kiboko wakiwa ndani ya bwawa hilo wakivua.

Alisema ajali hizo zimekuwa zikitokea kutokana na wavuvi kuvua kwenye mazizi ya viboko, wavuvi kutumia zana duni za uvuvi, kupungua kwa samaki katika bwawa hilo na wavuvi kufanya shughuli ya uvuvi nyakati za usiku ambapo viboko wanakuwa katika harakati za kutoka nje kutafuta chakula.

Scanned with CamScanner